OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI – KOROGWE

NAMBA ZA SIMU:

Mkuu wa Shule: 0769036380
Makamu Mkuu wa shule:0652448655
Makamu Mkuu wa shule:0710542504
Acakorogwesec2021@gmail.com

SHULE YA SEKONDARI
YA WASICHANA KOROGWE,
S. L. P. 155,
KOROGWE

18/05/2021

KUMB. Na. KGSS/A/10/33/VI/ 18/05/2021

Mwanafunzi……

……

S. L. P. . ……

…….

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KOROGWE MWAKA 2021/2022

1.0. Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **tano** Tahasusi ya …….. katika shule hii mwaka **2021/2022**. Shule ya sekondari ya Wasichana Korogwe ipo umbali wa Kilometa moja kutoka kituo cha mabasi cha mji wa Korogwe. Usafiri wa Bajaji/taxi unapatikana katika kituo cha mabasi cha Mji wa Korogwe. Nauli ni shilingi elfu moja (Bajaji) na elfu tatu (tax).

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ***05/07/2021*** Unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe **.....** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **.....**

2.0.Mambo ya kuzingatia

2.1.Sare za Shule

(a). Sare za shule zinashonwa shuleni ili kuleta mlingano. Gharama za sare ni kama ifuatavyo.

(i)	Sketi mbili- Orange	Sh. 40,000/=)
(ii).	Nguo za kazi	Sh.20,000/=
(iii).	Sweta	Sh.15,000/=
(iv)	T. Shirt moja	Sh. 7,500/= (Ukitaka mbili lipa sh.15000/=)
(vi).	Mashati mawili meupe	Sh. 16,000/= (Nusu kanzu 20,000/=

N.B Fedha za sare zitalipwa taslimu kwa fundi wa nguo anayepatikana shuleni.

(b). (i). Hijabu rangi nyeupe (tetron)
(ii) Sare ya viatu vya darasani ni viatu vyeupe au raba nyeupe ambavyo havina kisigino

(c). Sare ya michezo kwa shule hii ni kama ifuatavyo;
(i). T-sheti nyeupe isiyo na picha, mchoro wala maandishi
(ii). Bukta rangi yoyote.
(iii). Sketi fungi ya rangi ya zambarau (purple) ya kuvaa juu ya bukta.
(iv). Raba nyeupe au nyeusi

2.2 Ada na michango ya shule;

(a). Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/=.

(b). Michango inayotakiwa kulipwa na mzazi ni;

i. Sh.35,000/= Ada muhula wa kwanza

(ii). Sh. 5,000/= Kwa ajili ya tahadhari.
(iii). Sh. 6,000/= Kwa ajili ya kitambulisho.
(iv). Sh. 15,000/= Ukarabati wa samani.
(v). Sh. 20,000/= Mchango wa taaluma.
(vi). Sh. 10,000/= kukodisha godoro.
(vii). Sh. 10,000/= kwa ajili ya mahafali
(viii) Sh. 10,000/= Kwa ajili Huduma ya Kwanza
(ix) Sh. 25,000/= Ujenzi wa Uzio
(x) Sh. 2,000/= Kwa ajili Nembo ya Shule
(xi). Sh. 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa walinzi na wapishi.
(xii) Sh. 6,000/= Kwa ajili ya **Bima iliyoboreshwa**. Aliye na **bima ya afya** hahusiki alete kadi ya bima.

N.B.

1. ***Jumla ya fedha ya michango na ada ni shilingi 174,000/=. Michango hiyo na ada ya shule (2.2 a na b) ilipwe kwenye Akaunti ya shule namba 41501100013 NMB tawi la Korogwe na mwanafunzi aje na risiti ya malipo ya benki ikiwa imeandikwa jina sahihi la mwanafunzi.***

2. ***Fedha yote ya sare za shule (2.1 a) ilipwe shuleni kwenye ofisi ya malipo anakopatikana fundi wa kushona wakati mwanafunzi anaporipoti shuleni.***

3. ***Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na ream 2 za karatasi aina ya A4.***

2.3 Vifaa vya Usafi

(a) Tahasusi ya **CBG** na **PCM** walete **ufagio** wa **chelewa**, **jembe lenye mpini**, **kwanja** , **Hard broom na toilet brush**

(b) Tahasusi ya **PCB** walete **ufagio** wa **chelewa**, **jembe lenye mpini**, **kwanja** **na mopper**.

(c) Tahasusi ya **HGK** walete **ufagio** wa **chelewa**, **jembe lenye mpini**, **kwanja** , **Toilet Brush na soft broom**

(d) Tahasusi ya **KLF** walete **ufagio** wa **chelewa**, **jembe lenye mpini**, **kwanja toilet brush na soft broom**

(e) Tahasusi ya **HKL** walete **ufagio** wa **chelewa**, **jembe lenye mpini**, **kwanja, panga na soft broom**

(f) **HGL** walete **ufagio** wa **chelewa**, **jembe lenye mpini**, **kwanja, Squeezer na toilet brush**

2.4 Mahitaji Mengine

(i) Ndoo, sahani, kijiko na kikombe.
(ii) Picha tatu za passport size (mwanafunzi awe amevaa blouse nyeupe wakati wa kupiga picha), na za wazazi ambao watakuta kumtembelea.
(iii) Koti la mvua au mwamvuli.
(iv) Shuka mbili au zaidi za rangi ya pink na blanketi moja

(v) Sketi mbili za blue iliyokolea (dark blue) za kuvaliwa nje ya darasa mshono wake ni rinda boksi na ifike kwenye kiwiko cha mguu (nguo nyingine za nyumbani mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuzivaa, hivyo asizilete)
(vi) Taulo, malapa, mswaki, kanga/vitenge viwili,mto, nguo ya kulalia na mahitaji mengine muhimu ya mtoto wa kike.
(vii) Chandarua kimoja cha pembe nne..
(viii) Suruali ya blue na tracksuti ya kujikinga na mbu wakati wa kujisomea usiku.
(ix) Madaftali makubwa 14, kalamu za kutosha na mathematical set moja.
(x) Vitabu vya dini na mahitaji mengine ya dhehebu la mwanafunzi.
(xi) Barakoa za kitambaa cha cotton ni muhimu sana kuja nazo.

N.B. 1. Kwa wanaosoma somo la Chemistry waje na (Digital stop watch pamoja na **Scientific Calculator).**

***Kwa wanaosoma somo la Biology, mwanafunzi waje na Dissecting Kit*.**

3.0 Sheria na Kanuni Muhimi za Shule

3.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria namba 26 ya mwaka 1970. Aidha inazingatia miongozo yote ya Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi;

1) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
3) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (prep.)
4) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
5) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
6) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
7) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
8) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
9) Mwanafunzi atakapofika shuleni awe amekata nywele robo nchi na zisiwe zimewekwa dawa. Shuleni hakuna kusuka nywele.

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo
3. Kutoa lugha Chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
4. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
5. Uasherati na ushoga
6. Ubakaji
7. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, uvutaji wa Sigara, Cocaine, milungi, kubeli n. k.
8. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
9. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
10. .Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
11. Kudharau bendera ya Taifa
12. Kuoa au kuolewa
13. Kupata mimba, kutoa mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
14. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
15. Kukataa adhabu kwa makusudi

16. Mwanafunzi kumiliki simu ya mkononi, redio na pasi ya umeme au kifaa chochote kinachotumia umeme.
17. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

4.0 Mambo mengine muhimu

(a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada na michango na maelezo mengine yatolewayo na shule.

(d) Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

MZAZI TUNATEGEMEA SANA USHIRIANO WAKO.

"KARIBU SANA KOROGWE SEKONDARI

A M MAUKA
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA
KOROGWE

OFISI YA RAIS
LOCAL GOVERNMENT AND REGIONAL ADMINSTRATION
KOROGWE TOWN COUNCIL
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

KOROGWE GIRLS
SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 155,
KOROGWE.

DATE……

MEDICAL OFFICER,…….. GOVN. HOSPITAL,
……..

NAME OF PUPIL……..
Please examine the above named girl to ascertain her fitness for further studies.

……..

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA
KOROGWE

HEADMISTRESS

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by the medical officer)
I have examined the above named with regard to:
Skin…….
Eyes…….
Ears……..
Chest…….
Spleen……...
Abdomen……..
Urine…….
Stool…….
Hemoglobin…….....
Other diseases ……
……....

And I considered:

1. She is good health, free from infection diseases, worms, bilharzias and fit to go to school.
2. She is now fit to return to school having treatment for……
   ……
   NAME AND SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER DATE

And I considered:

3. She is now fit to return to school having checked for……
   ……
   …… ……. ……
   NAME AND SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER DATE

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA – KOROGWE

KOROGWE SEKONDARI
YA WASICHANA,
S. L. P. 155,
KOROGWE.

(C): FOMU YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA

SEHEMU A: Habari za Mwanafunzi.

1. Jina kamili……
2. Tarehe ya kuzaliwa……..
3. Wilaya alipozaliwa…….. Kijiji ……
4. Kukubali nafasi (Ijazwe na mwanafunzi)

BANDIKA PICHA KAMA ZA WATAJWA HAPO CHINI

PICHA YA MWANA FUNZI	PICHA YA MZAZI/ MLEZI 1	PICHA YA MZAZI/ MLEZI 2

AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi mwanafunzi …… nimeyasoma maagizo yote ya kujiunga na shule ya Sekondari ya Wasichana Korogwe na ninakubali kwa dhati kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na uletaji wa vifaa vinavyohitajika na kutii sheria zote za shule kama zilivyotolewa na uongozi wa shule. Nitakapokuwa shuleni Korogwe nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuzingatia yote ambayo wanafunzi wanatakiwa kutimiza katika suala zima la kupata Elimu ya kujitegemea.

Sahihi ya Mwanafunzi…… Tarehe……..

AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi mzazi/mlezi wa …….....naahidi kwamba nitatimiza wajibu wangu kwa mwanangu na kumsisitizia kufuata taratibu za shule kama ilivyoelekezwa na Uongozi wa shule , kumpa mwanangu malezi mema na kutoa ushirikiano kwa shule ili apate matokeo mazuri

1. Jina kamili la mzazi/mlezi……
2. Uhusiano na mwanafunzi mzazi ……..mlezi……
3. Kazi yake ……..……..
4. Anwani ya Mzazi/Mlezi…….……
5. Namba tatu za simu ikiwemo ya Mzazi/Mlezi na ndugu wa karibu wa Mwanafunzi

(1) ……(2) ……(3) …….……

Sahihi ya Mzazi/Mlezi…….. Tarehe……